**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA

**16 MEI, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 16 MEI, 2017

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## III. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**209. MHESHIMIWA DKT. PUDENCIANA WILFRED KIKWEMBE (KAVUU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imekuwa na dhana ya Ugatuaji Madaraka kwa Wananchi ili kurahisisha maendeleo hususani katika sekta za Afya na Elimu:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu mfumo huo kutokuwa na tija endelevu katika sekta hizo.

**210. MHESHIMIWA ENG. ATASHASTA JUSTUS NDITIYE (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kwa muda wa zaidi ya miaka miwili, Hospitali ya Wilaya ya Kibondo haina Mganga wa meno licha ya Hospitali hiyo kuhudumia Wagonjwa wengi kwa sasa ikiwemo Wakimbizi kutoka Nchi jirani ya Burundi:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Mtaalam wa meno katika Hospitali hiyo.

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI:

**211. MHESHIMIWA DANIEL EDWARD MTUKA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:- Eneo la Muhalala katika Wilaya ya Manyoni ni moja ya maeneo matatu yaliyoteuliwa na Serikali kujenga Vituo vya Ukaguzi wa mizigo katika barabara ya kati; Maeneo mengine ni Vigwaza Pwani na maeneo mawili yameshajengwa kimebaki Kituo cha Muhalala tu:-

(a) Je, ni lini Wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa tangu Mwaka 2012 watalipwa fidia;

(b) Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa mizigo Muhalala baada ya Kituo cha Vigwaza kukamilika.

**212. MHESHIMIWA MUSSA BAKARI MBAROUK (TANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:- Bandari ya Tanga siku hadi siku inafanya kazi chini ya kiwango:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kina, kuipanua na kuifanya bandari ya kisasa ili kuvutia wafanyabiashara kushusha mizigo yao na wasikimbilie Mombasa Kenya.

**213. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:- Katika Bunge la 10 Serikali iliahidi kufunga mtambo kwa lengo la kudhibiti takwimu za Simu za nje na ndani ili kudhibiti mapato ya Serikali:-

(a) Je, utekelezaji wa suala hilo umefikia wapi;

(b) Je, ni kiasi gani Serikali imekusanya tangu utaratibu huo uanze na kabla yake mapato yalikuwaje.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

**214. MHESHIMIWA FRANK GEORGE MWAKAJOKA (TUNDUMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Mji wa Tunduma una Vijana wengi wanaohitimu Kidato cha Nne lakini wanakosa nafasi za kuendelea na masomo ya Juu:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu kujenga Chuo cha Ufundi VETA ili Vijana wengi waweze kupata ujuzi na kujiajiri na kuongeza kipato chao.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

**215. MHESHIMIWA ESTHER MICHAEL MMASI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Kupitia fursa ya ujenzi wa Bomba la Mafuta Mkoani Tanga ni dhahiri kwamba Vijana takribani 15,000 watapata ajira kwenye mradi kwa upande wa Tanzania:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kuona kuwa Vijana wa Kitanzania wanapata ajira katika soko la Tanzania kupitia fursa hii ya Uwekezaji;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza Mtaala wa Mafuta na Gesi katika Mitaala ya VETA ili kuwajengea uwezo, maarifa na ujuzi vijana wa Kitanzania katika sekta hiyo muhimu.

**216. MHESHIMIWA PROF. NORMAN ADAMSON SIGALLA KING (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Utafiti uliofanywa na Serikali unaonyesha kuwa Mto Lumakali unaozalisha maji katika Wilaya ya Makete unaweza kuzalisha *Megawats* 640 za umeme na hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya ya Makete inapata mvua kwa miezi nane (8) kwa mwaka:-

Je, ni lini ujenzi wa Bwawa ambao ni mpango wa Serikali wa tangu mwaka 2005 utaanza ili kusaidia kujenga uchumi wa kudumu huko Makete, Mkoa wa Njombe na Mbeya kwa ujumla.

**217. MHESHIMIWA SUSANNE PETER MASELLE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, kwa nini Serikali imewanyang'anya ajira Vijana waliokuwa wamejiajiri kwenye machimbo ya Ishokulahela na baadae ikaamua kubadili umiliki wa leseni kwa siri.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

**218. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kumekuwa na tatizo kubwa sana la ukosefu wa maji safi na salama katika Mkoa wa Simiyu pamoja na Wilaya zake ambazo ni Bariadi, Itilima, Busega, Maswa na Meatu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji Wananchi wa Mkoa wa Simiyu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI

## WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**DODOMA** — **DKT. T. D. KASHILILAH**
**16 MEI, 2017** — **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA